

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na.MTC/I. 20/2.VOL.I/58

05/03/2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KIBARUA WA MKATABA KWA KAZI YA UDEREVA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako, anapenda kuwatangazia wataanzania wote wenye sifa tajwa hapo chini, kuomba nafasi ya kibarua wa mkataba kwa kazi ya udereva.

DEREVA DARAJA LA II: NAFASI TANO (5) (DRIVER II)

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe na cheti cha kidato cha nne (FORM IV)
2. Awe na Leseni ya Udereva Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari amabayo amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
3. Awe na cheti cha mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na VETA au NIT au Chuo kingine kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU

1. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
2. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
3. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
4. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
5. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
6. Kufanya usafi wa gari na,
7. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na msimamizi wake.

NGAZI YA MSHAHARA

TGS B₁ TSHS. 450,000/= Kwa Mwezi.

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE AMBAYO NI YA LAZIMA KUZINGATIWA

1. Mwombaji ni lazima awe ni Raia wa Tanzania.
2. Awe hajawahi kufungwa kwa makosa ya jinai.
3. Maombi ni lazima yaambatishwe na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa, Kitambulisho cha Uraia(NIDA) au namba ya NIDA (Kwa wasio na vitambulisho vya NIDA) na kivuli cha vyeti kuhitimu Elimu ya Sekondari na vyuo vya mafunzo/taaluma vinavyotambuliwa na Serikali.
4. Awe na Umri usiozidi miaka 45.
5. Maombi lazima yaambatishwe na picha 2 za Passport Size za hivi karibuni.
6. Maombi lazima yaambatanishwe na CV (Curriculum Vitae) (Wasifu).
7. Awe na umri zaidi ya miaka 18
8. Hati za matokeo za kidato cha nne na hati za vyeti vya taaluma havitapokelewa.
9. Watakaoitwa kwenye usaili watajigharamia wenyewe.
10. Maombi yanaweza kuandikwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili au Kingereza.
11. Awe tayari kufanya kazi eneo lolote atakalopangiwa ndani ya Halmashauri ya Mji Makambako.
12. Awe na wadhamini wawili (2) ambao ni watumishi wa Serikali.
13. Barua za wadhamini zipitishwe kwa waajiri wao.


MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO:-

MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI,
S.L.P 405,

MAKAMBAKO.

MWISHO WA KUTUMA MAOMBI NI TAREHE 15/03/2024

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-


Kenneth K. Haule
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
MAKAMBAKO

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI

Halmashauri ya Mji Makambako, Mtaa wa Sigrid, Barabara kuu ya Njombe, S.L.P 405
Makambako, Njombe, Nukushi Na: 026-2968891, Simu Na: 026-2968892,
Barua Pepe: td@makambakotc.go.tz, Tovuti: www.makambakotc.go.tz